TANGAZO LA SERIKALI NA.146 la tarehe 3/3/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI

(SURA 355)

# AMRI

*(Imetolewa Chini ya Kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA ZANKA YA MWAKA, 2023.

Jina:

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Eneo la Zanka ya mwaka, 2023

Utangazaji wa Eneo la Upangaji Sura (355)

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (mpango wa urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpangokina wa eneo

3. Mipango ya jumla na kina ya eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi.

______

JEDWALI

_______

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*
Eneo urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatavyo:-

"Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba ZK1 yenye majira - nukta 806316.271MS, 9354844.258KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa KZ98$^{0}$10''MS kwa umbali wa kilomita 1.37 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba ZK2 yenye majira - nukta 807680.584MS ,9354648.067KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki kwa kukatisha barabara ya Arusha - Dodoma katika uelekeo wa MS109$^{0}$ 24''kwa umbali wa kilomita 0.97 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba ZK3 yenye majira - nukta 807869.856MS, 9353692.931KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa KS134$^{0}$ 38''MS kwa umbali wa kilomita 2.43 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba ZK4 yenye majira - nukta 806501.594MS, 9351681.971KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini katika uelekeo wa KS163$^{0}$27'' kwa umbali wa kilomita 0.76 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba ZK5 yenye majira - nukta 805908.447MS, 9351198.831KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Magharibi katika uelekeo wa KS91$^{0}$54''MG kwa umbali wa kilomita 0.72 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba ZK6 yenye majira - nukta 805433.314MS, 9351747.526KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi kwa kukatiza barabara ya Dodoma – Arusha katika uelekeo wa MG169$^{0}$48'' kwa umbali wa kilomita 1.40 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba ZK7 yenye majira nukta 804342.373MS, 9352633.091KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa KS102$^{0}$07''MG kwa umbali wa kilomita 0.88 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba ZK8 yenye majira - nukta 804737.572MS, 9353421.887KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa KZ158$^{0}$14''MG kwa umbali wa kilomita 2.12 hadi ulipoanzia."

Dodoma,
6 Februari, 2023

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*